



OFISI YA WAZIRI MKUU SERA,BUNGE NA URATIBU

IDARA YA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UTENDAJI WA SERIKALI

IDARA YA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA UTENDAJI WA SERIKALI

Lengo: Kufuatilia na kutathmini utendaji wa Serikali kwa ujumla.

Idara kinapewa mamlaka ya kufanya kazi zifuatazo:

- i. Kutathmini utendaji wa Wizara, Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- ii. Kufuatilia na kutathmini mipango ya vipaumbele;;
- iii. Kuendeleza na kudumisha mfumo thabiti wa kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini
- iv. Kuwa msimamizi wa Sera ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Serikali;
- v. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Tathmini wa Taifa (NEP);
- vi. Kuendeleza na kufuatilia utekelezaji wa Viashiria Muhimu vya Utendaji kwa kushirikiana na Wizara za Sekta;
- vii. Kuratibu Ufuatiliaji na Tathmini ndani ya serikali;
- viii. Kutathmini ufanisi wa mikataba ya maelewano baina ya taasisi;; na
- ix. Kuandaa taarifa za utendaji wa Serikali kwa vipindi maalum

Idara hii ina Sehemu kuu mbili:

- i. Sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Wizara; Na
- ii. Sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utendaji wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

Sehemu ya Utendaji wa Wizara inafanya kazi zifuatazo;

- i. Kufuatilia na kutathmini utendaji wa Wizara;
- ii. Kufuatilia na kutathmini utendaji wa Vitengo/sehemu za Ufuatiliaji na Tathmini katika wizara zote;
- iii. Kuandaa na kutekeleza Mpango wa Tathmini ya Taifa (NEP);
- iv. Kuendeleza na kudumisha mfumo thabiti wa kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini
- v. Kuratibu na kuwianisha mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini katika ngazi ya Taifa;
- vi. Kutathmini ufanisi wa makubaliano ya mashirikiano, makubaliano na mifumo ya shughuli za pamoja, mipango na programu;
- vii. Kuandaa na kufuatilia utekelezaji wa viashiria vya utendaji muhimu wa Taifa kwa kushirikiana na wizara za sekta; Na
- viii. Kuandaa maandiko na maelezo mafupi juu ya utendaji na kusambaza taarifa.

Kwa maelezo zaidi wasiliana:

ofisi ya waziri mkuu
S.L.P 980 dodoma
Tel: +255-22-212215
Fax: +255-22-21-21826
Barua pepe:ps@pmo.go.tz